



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UAMUZI WA RUFAA ZA
WAGOMBEA UDIWANI

Dar es Salaam, 15 Septemba, 2020

Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake cha tarehe 14 Septemba 2020 imepitia, imechambua na kuzifanyia uamuzi rufaa za wagombea Udiwani zilizowasilishwa na wagombea kupitia kwa Wasimamizi mbalimbali wa Uchaguzi nchi nzima.

Rufaa hizo zimewasilishwa chini ya kifungu cha 44 (5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 ambacho kinatoa fursa kwa wagombea wa Udiwani kukata rufaa wanapokuwa hawajaridhika na uamuzi wa Wasimamizi wa Uchaguzi kutokana na pingamizi zilizowasilishwa.

Aidha, chini ya kanuni ya kanuni ya 30 (3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Madiwani) za mwaka 2020, Tume inaweza kukubali au kukataa rufaa hizo.

Katika kikao hicho, Tume imezipitia, kuchambua na kuzifanyia uamuzi jumla ya rufaa 87 za Wagombea Udiwani, kama ifuatavyo:-

- i. Imekubali rufaa 47 na kuwarejesha wagombea Udiwani katika orodha ya wagombea Udiwani. Rufaa hizo ni kutoka kwenye Kata za Mwanhuzi

(Meatu), Kondoa Mjini (Kondoa Mjini) Msasa (Handeni Mjini), Bunju (Kawe), Bunju (Kawe), Ipagala (Dodoma Mjini), Isuto (Mbeya Vijijini), Iwiji (Mbeya Vijijini), Kichangani (Morogoro Mjini), Kimara (Ubungo), Likongowele (Liwale), Matumbulu (Dodoma Mjini), Nsalala (Mbeya Vijijini), Ulenje (Mbeya Vijijini), Muriti (Ukerewe), Ruvu (Same Magharibi), Kisutu (Bagamoyo), Majimaji (Tunduru), Mtibwa (Mvomero), Unyanga (Singida Mjini) na Kagondo (Bukoba Mjini)

Nyingine ni Kaloleni (Moshi Mjini), Mlabani (Kilombero), Fukayosi (Bagamoyo), Igurwa (Karagwe), Kauzeni (Morogoro Mjini), Maisaka (Babati Mjini), Ndama (Karagwe) Olorien/Magaiduru (Ngorongoro), Kilole (Lushoto), Ngwelo (Lushoto), Hondomairo (Kondoa Mjini), Nyasiura (Bunda Mjini), Ikhanoda (Singida Kaskazini), Nyabiyonza (Karagwe), Kibiti (Kibiti), Ruvu Remit (Simanjiro), Ihanda (Karagwe), Mabanda (Handeni Mjini), Bungu (Kibiti), Kapala Msenga (Mpanda Vijijini), Businde (Kyerwa), Igoma (Mbeya Vijijini), Likongowele (Liwale), Shizuvi (Mbeya Vijijini), Mlembwe (Liwale) na Tambukareli (Dodoma Mjini).

- ii. Imekataa rufaa **30** za wagombea Udiwani ambao hawakuteuliwa. Rufaa hizo ni kutoka kwenye Kata za Tongwe (Muheza) Kiomboi (Iramba Magharibi), Jangwani (Ilala), Mlali (Mvomero), Kiloleni (Sikonge), Mbasu (Kilombero), Dakawa (Mvomero), Dakawa (Mvomero), Jibondo (Mafia), Kigombe (Muheza), Buhumbi (Magu), Mlali (Mvomero), Olbalbal (Ngorongoro), Kidete (Kilosa), Bugene (Karagwe), Kihanga (Karagwe), Mabogini (Moshi Vijijini), Hemtoye (Mlalo), Mlali (Mvomero), Mbaramo (Mlalo), Mbaru (Mlalo), Okaoni (Moshi Vijijini), Nangando (Liwale),

Magomeni (Kinondoni), Kitangiri (Ilemela), Dareda (Babati Vijijini), Iganjo (Mbeya Mjini), Ipembe (Singida Mjini), Kilema Kaskazini (Vunjo) na Nyamhongolo (Ilemela).

- iii. Imekataa rufaa 10 za kupinga wagombea Udiwani walioteuliwa. Rufaa hizo ni kutoka kwenye Kata za Forest (Mbeya Mjini), Mabatini (Mbeya Mjini), Mkowe (Kalambo), Kaloleni (Moshi Mjini), Mwangoi (Mlalo), Malibwi (Lushoto), Kwa Kilosa (Iringa Mjini), Kihesa (Iringa Mjini), Nzubuka (Tabora Kaskazini) na Ihumwa (Dodoma Mjini).

Idadi hii inafanya jumla ya rufaa za wagombea Udiwani zilizotolewa uamuzi kufikia 331. Tume itaendelea kutoa matokeo baada ya usajili na uchambuzi wa rufaa hizo kila siku. Wahusika wa rufaa hizo watajulishwa kwa barua juu ya uamuzi wa Tume.



Dkt. Wilson Mahera Charles

MKURUGENZI WA UCHAGUZI
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI